Haya ni Mahindi, sio Makana

(Hotuba kuzindua Kitabu Makuadi wa Soko Huria)

na

Issa G. Shivji (Prof.)
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
issashivji@gmail.com

Jina: Makuadi wa Soko Huria
Mwandishi: Chachage Seithy L. Chachage
Kurasa: 287
Mwaka wa Uchapishaji: i: 2002
Mchapishaji: E&D Ltd.

Ni ukweli usiopingika kwamba mwandishi wa riwaya, kama walivyo wasanii wengine, ni kielelezo ni kioo cha jamii. Katika maandishi yake jamii hunung'unika na kuwaza, hufurahia na kusikitika, hujikejeli na kujikosoa. Riwaya ndiyo inayoweka wazi siri za jamii, inaanika hadharani aibu za waheshemiwa na kusema kwa uwazi na ukweli yale yasiyoosemeka. Hohehahe, ambao hudharauliwa na kupuuzwa na waheshemika, ndio huwa mashujaa wa riwaya, kwani hupata nafasi stahiki, kwa sababu wao ndio siku zote hubeba mzigo wa maendeleo ya jamii pamoja na maisha ya anasa waishiyo waheshemika.

Lakini sio kila mwandishi wa riwaya huwa kielelezo cha aina hiyo. Ninayemsimulia mimi ni mwandishi stadi wa riwaya, siyo lazima awe mwandishi mwenye msimamo wa kimaendeleo, kijamii au kisiasa, wala siyo mwandishi aliyesoma na kubobea katika fani ya fasihi. Inatosha kama akiwa mwandishi stadi, mwandishi anayekereketwa na kero za jamii yake, anayetambua upeo wa mwanadamu, mwanadamu yeyote yule.

Tuna mfano mzuri tu wa mwanafasihi kama huyo. Namwazia Ebrahim Hussein. Nimemfahamu Ebrahim kwa muda mrefu tu tangu nikisoma shule ya sekondari ya Tambaza, wakati ule ilikuwa shule ya Agakhan - kwa jina na kwa milki! Bila ya kuyapuuza maoni na msimamo wake, ningependa kusema, kwa heshima yote anayostahili, kwamba, kwa maoni yangu, Ebrahim hawezi kuhesabiwa kati ya wale wenye msimamo na mwelekeo wa kimapinduzi au hata mkereketwa wa wanyonge.

Lakini ukweli ni kwamba, kwa kuwa yeye ni msanii stadi, riwaya zake na michezo yake huwakilisha kwa ufasaha na ubinadamu, hali, ushujaa na msimamo wa wanyonge, tena kwa usanii wa hali ya juu.

Ningependa kunukuu shairi lake juu ya Numeiri aliyetawala Sudan kwa mabavu mnamo miaka ya 80.

Numeiry
Shairi anapenda
Lakini lile linalomsifu.
Kawanda anawanda
Hasa akisikia maafu
Vita, njaa ya watoto wafu.
Elimu ambayo ni sakafu
Ya maisha, kwake ni ubabaifu.

Lakini Ebrahim Hussein amesomea fasihi, yeye ni mtaalamu katika mambo ya riwaya na michezo na sanaa ya maandishi. Mwandishi wa riwaya ya ***Makuadi wa Soko Huria***, Chachage Seithy Chachage, siyo mtaalam wa fasihi, wala hakusomea fani hiyo. Kitaaluma, fani yake ni sosiolojia. Lakini, kamaradi Chachage amekerwa na unyonge na dhuluma katika jamii yake, ameteswa na ukandamizwaji wa watu na amefarijika na ujasiri wa umma. Chachage ameaibishwa na makuadi ambao hunadi nchi yao, taifa lao, ardhi yao, mama yao kwa bei yoyote ile katika soko la mabeberu. Amekerwa vya kutosha, kiasi kwamba amejikuta anaandika riwaya. Hakuwa na njia nyingine ya kuwasilisha ujumbe wake, kero zake wala kutangaza matumaini yake na imani yake: imani yake isiyotetereka kuhusu umma wa wanyonge na uwezo wao wa kujikomboa kutoka mfumo-dhuluma na kujenga jamii yenye usawa, haki, heshima na ubinadamu. Chachage alihisi kwamba makala hayatoshi - ingawa ameandika, na anaendelea kuandika makala ya kutosha, tena mazuri tu; akaona mihadhara haifui dafu, ingawa michango ya Profesa Chachage katika semina na warsha hujulikana kwa ukweli na ukali wake.

Hata hivyo, hakukata tamaa. Mwanaharakati halisi kamwe hawezi kukata tamaa. Katika vita dhidi ya dhuluma, ikiwa hali hairuhusu, anarudi nyuma kidogo, lakini kamwe hasalimu amri. Na Chachage ni mwanaharakati. Hawezi kusalimu amri, na, nina matumaini kwamba hatasalimu amri … . Ataendelea kutumia silaha yake kubwa:

kalamu. Safari hii amejikuta anaandika riwaya, anaandika kuhusu Binti Wenga, siyo ***first lady***, wala siyo mwenzake mwanachuo, wala siyo mtu mashuhuri kisiasa, wala siyo jina lililoko katika majuzuu ya historia. La hasha. Binti Wenga siyo kati ya hao watu mashuhuri, watu wa 'society' ambao 'sanamu' zao tunaziona kila siku katika televisheni, wakiwa ama wanatoa nasaha zao juu ya mambo ambayo wao wenyewe ni wakiukaji wakubwa au wakiwa wanakunywa na kula na wenzao 'watandawazi'. Bi. Wenga siyo mtu binafsi. Bi. Wenga ni miongoni mwa wale wanadamu ambao hukuza na huheshimu ubinadamu wao kiasi kwamba kwao, kila siku ya Bwana ni mapambano, mapambano ya kujikimu, mapambano ya kulinda uhuru wao, ubinadamu wao, na wa jamii yao.

Chachage anaandika, anaimba, anatangaza harakati za akina-Wenga. Anasheherekea ujasiri wao, anatunza heshima zao, anajifunza na anachota bila kikomo kutoka katika kisima cha busara zao. Riwaya ya Chachage haina mashujaa, mashujaa wa Chachage ni watu wenyewe, watu wa kawaida tu, hohehahe - wakiwemo wazee wa Delta ya Rufiji, akina-Mzee Miraji na Mzee Mrisho. *Makuadi wa Soko Huria* haina wasomi na wataalam, wataalam wa siasa na wataalam wa historia. Siasa ya wana wa Rufiji ni hekima yao, upeo wao uliokua, na unaoendelea kukua, kutokana na uzoefu wa karne za mapambano. Historia yao ni kumbukumbu zao, kumbukumbu ambazo hazina utata wala ubishi kwani zimewekwa na kutunzwa kama sehemu ya maisha yao, ni kiini cha utamaduni wao.

Katika hili, yaani, katika kuandika riwaya isiyokuza ushujaa wa mtu au watu binafsi, Chachage amemkaribia mwandishi mashuhuri wa kimapinduzi, Maxim Gorky. Kwangu mimi, hili tu linanitosha kumweka Chachage katika orodha ya wasanii stadi wa Tanzania, na wa Bara la Afrika.

Lakini kuna mengi mengine katika masimulizi haya. Siwezi, wala sitaki, kutoa muhtasari. Riwaya husomwa, na husomwa tena na tena, na hapana budi isomwe ilivyo, ndio msomaji apate utamu wake. Na kama masimulizi yenyewe ni matokeo ya kalamu ya Chachage, basi msomaji hana budi kusoma kila ukurasa, ili, pamoja na kufaidi utamu wake, aukwaruzwe pia na ukali wa kalamu yake. Hata hivyo, ninashindwa kujizuia kumzungumzia mwenzi wangu wa kitabaka, Mjuba.

Mjuba ni mwandishi wa habari na mwanaharakati, ni mhusika mmojawapo katika *Makuadi …* . Mjuba na wenzake, wakifadhiliwa na wahisani, wanafunga safari ya

Delta ya Rufiji kuchunguza mradi wa kufuga kamba. Bwana Mooney ndiyo mwekezaji mashuhuri wa mradi huo.

Mjuba ni mwanamapinduzi, au, anajihisi yeye ni mwanamapinduzi. Mapambano yake ni yale ya kujinyonga kitabaka, kwa maana ya Cabral. Kwa upande mmoja, kuna hulka ya tabaka lake la kibwenyeye ("petty bourgeoisie") - uchu wa kutajirika haraka-haraka, wa kupanda ngazi kwa mkupuo, kulimbikiza mali, na kuishi maisha manono ya anasa. Kwa upande mwingine, kuna mvuto wa kuleta mabadiliko katika jamii, iwe jamii yenye usawa na haki. Pande hizi mbili ndizo nafsi mbili za tabaka la kibwanyeye ambazo daima huvutana. Mwenerumango ni miongoni mwa wanahabari, lakini kwa siri ni kibaraka wa Lupocho. Lupocho ni tajiri wa Rufiji, ingawa ni tajiri-mchwara kwa sababu hatimaye, bepari mwenye kauli nzito na uamuzi wa mwisho ni mwekezaji Mooney.

Nje, Mjuba anapambana na adui, dola na ubeberu. Lakini mapambano ya kitabaka yana sura mbalimbali. Ndani, katika familia yake mwenyewe, yuko mwenziwe aliyemuoa na kuzaa naye, kwa jina, Salama, au Mama Nkrumah. Mjuba, kama kawaida ya "wanamapinduzi wa mezani" (alivyokuwa anawaita Philip O'chieng, 'revolutionaries at the (bar)counter!), alikuwa anatumia muda wake mwingi baada ya kazi kujumuika na wanahabari wenzake, wakipiga soga na kudadisi jamii yao, hali ya wanyonge na matumaini ya mapinduzi. Matokeo yake, hali ya familia ilididimia. Mjuba alikuwa anachelewa kurudi nyumbani akiwa amepanda dala-dala wakati wenzi wake kitabaka wanatamba na magari ya anasa.

Salama akaasi. Uasi wa Salama ni kuokoka. Katangaza *Ilani ya Uasi* kwa maneno haya:

> Imeandikwa, tusile nira na watu wasiomcha Bwana. Itabidi ubadili maisha yako. Hizi taabu zote na hii hali ya kutoendelea kimaisha imetokana na madhambi yetu. Mimi nimezaliwa upya. Bila hata wewe kuzaliwa upya, nadhani maisha yetu ya ndoa hayatakuwa mazuri. Kama hivi leo umekunywa pombe, basi ujue kwamba hakuna haki ya unyumba! [uk. 33]

Naam, adhabu imetendeka, adhabu yenye madhara makubwa kuliko zile zitolewazo na dola. Mjuba kajizamisha katika pombe ili kupoteza mawazo. Pamoja na ustaarabu na uwajibikaji wake wa hali ya juu, kuteremsha porojo hadharani, akiwa amelewa, halikuwa tena jambo geni kwa Mjuba.

Ndugu yangu Chachage, hapo umepatia vizuri mtanziko (*dilemma)* wa mwanamapinduzi wa kibwaenyeye, hali ambayo tunajikuta tumo wengi wetu wenye msimamo wa kimaendeleo.

***

Kwa upande mwingine, kuna Sifuni, pia ni mwanahabari, pia ni mwanamke mwenye msimamo wa kimapinduzi. Sifuni aliolewa na Oscar kwa sababu alikuwa anampenda. Oscar ni kijana wa kawaida kabisa. Anatamani maisha mazuri. Akapelekwa huko Zanzibar kikazi. Akamtia mimba mtoto wa Waziri. La haula! Akajikuta anabadili dini, akawa Hassan, ili afunge ndoa na huyo mtoto wa Waziri. Akautelekeza uhusiano wake na mkewe Sifuni.

Mjuba na Sifuni wote wakawa wapweke! Fikra zao za kimaendeleo, bila shaka, zikawajumuisha Mjuba na Sifuni ingawa upekwe wao ndio uliwawezesha kuwasiliana kimoyo. Swali: kipi kati ya mapenzi ya mapinduzi na mapenzi ya kimwili, kitashinda? Kwani ni lazima, liwe moja kati ya mawili? Kwani, mapinduzi ni mapenzi mbadala?

Sina jibu, wala sina uhakika kama riwaya tunayoizindua ina majibu. Sio lengo la riwaya kutoa majibu. Lengo kuu la riwaya ni kudadisi, na kushtua jamii kujidadisi.

***

Nimetumia muda kidogo kugusia kijisehemu kidogo tu cha *Makuadi wa Soko Huria*. Nimegusia hasa mapambano ya ki-nafsi ya akina-Mjuba kwa sababu ninaelewa kwamba tuliokusanyika hapa, sijui wangapi - (sina haki ya kukisia wala kubuni) - tunashiriki na Mjuba katika hulka na mitanziko (*dilemma)* ya mwanamapinduzi itokanayo na tabaka la kibwenyeye. Sikuwagusia makuadi, akina-Lupocho na Mwenerumango, vibaraka vya Mooney. Sina haja ya kupoteza muda wangu kwao, isipokuwa wapo katika jamii yetu. Na ikiwa wataisoma riwaya hii, watajiona uchi kupindukia katika kioo cha *Makuadi*.

Wajisalimishe … ! Kwani wana wa Rufiji - akina Binti Wenga, na Amina, na Mzee Miraji na Mzee Mrisho - waliolea Kinjekitile na Bibi Titi Mohamed, wako mbioni kuwalea akina-Mjuba, na akina-Sifuni na akina-Fidelis.

Makuadi wa soko huria, jisalimisheni, damu ya wakombozi imechemka!.

***

Nilianza na Ebrahim Hussein. Nimalizie na Ebrahim Hussein. Sisi wasomi tuna wajibu, sio tu wa kuwakilisha, kimawazo na kivitendo, msimamo na mwelekeo wa wanyonge, bali pia kuchambua na kuonyesha unafiki wa mawazo na mwelekeo wa matabaka-tawala. Ebrahim Hussein, ingawa yeye mwenyewe hatambui dhana ya tabaka, anadhihirisha unafiki wa mawazo ya matabaka-tawala anapoimba, na ninanukuu:

Ninajifunza
Usiku na mchana
Kupokea makana
Na kusema haya ni mahindi.

Ahsanteni.

Issa Shivji
Oktoba 17, 2002